Mwongozo Wa Mwalimu

4

# Majaribu

## Kujiandaa na kukabiliana na Majaribu



MVMM

Mafunzo ya Vikundi
Yanayohusu Maisha Mapya

# Majaribu

## Kujiandaa na kukabiliana na Majaribu

Kimeandikwa Na David Batty

Mwongozo Wa Mwalimu

Toleo la Tano

MVMM
Mafunzo ya Vikundi
Yanayohusu Maisha Mapya

# Majaribu

## Kujiandaa na kukabiliana na Majaribu

Kimeandikwa Na David Batty
Mwongozo Wa Mwalimu
Toleo la tano

Maandiko yanayotumiwa katika kitabu hiki yametoka kwa:

MAANDIKO: Biblia Takatifu (Union Version). Toleo La 1952, 1974, 1976, 1978. BST, BSK. Yametumiwa Kwa Ruhusa Maalum.

Tafsiri Ya Lugha Rahisi (TLR) itakayofanywa na mtafsiri ili kuleta maana halisi kama inavyosomeka katika lugha ya Kiingereza.

HakiMiliki © 2023, Teen Challenge USA.

Vitabu vya Mwalimu na kila kitu cha mwanafunzi vinavyohusiana na masomo haya ya *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya, k*inatawaliwa na Sheria za HakiMiliki. Mpango maalum umefanywa ili kufasiri masomo haya kwa lugha hii yaKiswahili. Masomo haya yanaweza kuchapwa na kupewa wengine kwa ajili ya matumizi katika huduma za Teen Challenge na zinazofanana nazo, katika makanisa ya mahali pamoja, shule na mashirika mengine na hata watu binafsi. Pia, yanaweza kupatikana kutoka kwa mtandao kwenye tovuti hii: www.iTeenChallenge.org lakini, yasiuzwe. Yatolewe bila malipo. Kwa wanaotaka kuchapisha na kuuza, wapate ruhusa kwa maandishi kutoka Global Teen Challenge.

Kwa mara ya kwanza, somo hili lilichapishwa kwa Kiingereza kwa jina lifuatalo: *Temptation, 5th edition*

Somo hili ni sehemu ya mfululizo wa masomo yaitwayo *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* vinatawaliwa ili kutumiwa makanisani, mashuleni, katika huduma gerezani, huduma za Changamoto Kwa Vijana, na huduma zingine kama hizo zinazofanya kazi na Wakristo Wapya. Vile vile kuna vifaa vingine vinavyopatikana kwa ajili ya mafunzo haya, kama kitabu cha kumwongoza mwalimu, cha kumwongoza mwanafunzi, kitabu cha kuongoza mafunzo cha mwanafunzi, mtihani, na cheti. Ukitaka habari zaidi juu ya masomo haya, wasiliana na:

Global Teen Challenge
PO Box 511
Columbus, GA, 31902 USA
Barua Pepe:gtc@globaltc.org
Tovuti: www.globaltc.org na
www.iTeenChallenge.org

MVMM
Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya

Mwaka wa Mwisho Kuhakikiwa: 08-2023

# Majaribu

Majaribu yatakuwa sehemu ya kawaida sana kwa maisha ya kila Mkristo.
Kusudi kuu la kozi hii ni kumwonyesha Mkristo mpya hatua za kukabiliana na majaribu.

1

### Sura ya 1. Majaribu maishani mwa Mkristo mpya

Tuchunguza jaribu ni nini na jinsi linavyoingiliana na maisha ya Mkristo. Tunapaswa kuwa makini sana ili kufahamu mahitaji na haja katika maisha yetu ambayo yanayohusiana na sehemu zinazokabiliwa na majaribu.

2

### Sura ya 2. Mchakato wa kuyashinda majaribu

Sura hii inahusika na hatua kadhaa unazoweza kuchukua unapokabiliwa na majaribu.

3

### Sura ya 3. Jinsi ya kujitayarisha kwa majaribu

Sura hii inazungumzia hatua ambazo mtu anaweza kuchukua ili kujiandaa dhidi ya majaribu. Tunachunguza jinsi Wakristo wanavyoweza kumkaribia Mungu na kutimiza mahitaji yao kwa njia za Mungu.
Pia tunaangalia jinsi tunavyoweza kuelekeza tamaa zetu kwa njia ambazo zinampendeza Mungu. Pia tumejumuisha majadiliano jinsi baadhi ya majaribu yanaweza kuzuiwa.

4

### Sura ya 4. Kuelewa kufeli na kukabilina nako kwa njia ya Mungu

Wakristo wapya hawataepuka kuingia kwa baadhi ya majaribu na dhambi. Tunachunguza kile kinachotokea katika uhusiano wetu na Mungu tunapofanya hivi, na tunajadili kile tunapaswa kufanya baada ya kuanguka kwa majaribu.

## Yaliyomo Katika Mwongozo Huu Wa Mwalimu

Kitabu hiki kina sehemu nne. Kila sehemu imeanza kwa ukurasa wenye rangi ya njano, ambao ni ukurasa ulio na jina la mada.

1. Mipango Ya Mwalimu ya Kufundishia Somo
2. Mwongozo Wa Mwanafunzi
3. Mwongozo Wa Somo
4. Mtihani Wa Mwanafunzi Na Cheti Cha Somo

Maelezo ya jinsi ya kutumia kila sehemu yanapatikana mara tu baada ya utangulizi wa ukurasa unaofuata.

# Utangulizi

Hili ni somo moja katika mfululizo wa masomo ulioandaliwa kwa ajili ya kuwafundisha Wakristo wapya. Tunaamini kwamba lipo hitaji kubwa sana siku hizi la kuwasaidia Wakristo wapya ili wahusishe mafundisho ya Kristo na maisha yao ya kila siku kwa vitendo. Mafundisho haya pia yanaweza kutumiwa vizuri sana kwa ajili ya huduma kwa vijana kanisani na watu wazima wanaotamani kufanya Ukristo kuwa sehemu ya maisha yao kila siku.

Kusudi kubwa la somo hili na mfululizo mzima wa *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* ni kuwatambulisha Wakristo wapya kwa maswali muhimu yanayohusu maisha. Hatujaribu kuwapa mafundisho yatakayokuwa ndiyo mwisho kuhusu mada husika.

Kamati ya Mtaala ya Huduma ya Teen Challenge Marekani, ina mpango wa kuendelea kupitia upya na kufanya marekebisho kwa masomo haya. Tunakaribisha mawazo yoyote au hoja za kutusaidia kuyaboresha.

## Jinsi ya kutumia Mwongozo huu Wa Mwalimu

### 1. Mipango Ya Mwalimu ya Kufundishia Somo

Kurasa za kwanza katika sehemu hii zinatoa mtazamo wa somo zima kwa ufupi.

Ukurasa unaofuata utakuwa ni nakala ya ***Orodha Ya Kazi Za Darasani***. Hii orodha inaonyesha wakati ambapo kila zoezi katika Mwongozo wa Somo linatakiwa kukamilishwa, na wakati kila chemsha bongo na mtihani zitatolewa. Kila mwanafunzi anapaswa kupewa habari stahiki kwa ajili ya ukurasa huo mwanzoni mwa kila somo. Kitabu hiki cha Mwongozo wa Somo tayari kina nakala isiyoandikwa chochote ya fomu hiyo, kwenye jalada la nyuma upande wa ndani.

Kitakachofuata ni mipango kwa ajili ya kufundishia kila somo. Hiyo yote ina kitu kinachoitwa Kweli Kuu ya Kibiblia pamoja na Mstari Mkuu. Hivyo vitu viwili vinaweza kutolewa mwanzoni mwa kipindi cha darasa. Pia vinasaidia kufanya mjadala ulenge yanayotakiwa kwa wakati wote.

Chini ya Kweli Kuu ya Kibiblia na Mstari Mkuu, kuna maelezo machache jinsi ya kufundisha somo lenyewe. Mara nyingi, marejeo yanaelekezwa kwa Mwongozo wa Mwanafunzi au kwa Zoezi linalopatikana katika Mwongozo wa Somo.

Kila somo humalizika kwa shughuli ya kufanya katika "Kufanyia Kazi Somo Maishani." Umuhimu wa kipengele hiki hauelezeki. Wakristo wapya wanahitaji mwongozo ulio wazi kuhusu jinsi ya kuanza kufanyia kazi mafundisho haya katika maisha yao ya kila siku. Hakikisha kwamba una toa nafasi ya kutosha ili kuwasaidia wanafunzi wako kuanzisha shughuli hii.

Mwisho wa kila mpango wa kufundishia somo kuna orodha ya kazi za wanafunzi kufanya.

Mengi katika masomo haya yalikusudiwa kuwa na vipindi vitano vya darasa, kila kimoja kikidumu kwa saa moja. Kipindi cha mwisho darasani ni kwa ajili ya mtihani. Masomo yote 14 katika mfululizo huu yanaweza kukamilishwa katika kipindi cha miezi kati ya mitatu hadi

minne, kama darasa litakutana kwa siku tano katika wiki. Ikiwa unafanya darasa kwa saa moja tu kwa juma, unaweza kukamilisha somo moja kwa mwezi – na mfululizo wote kwa kama mwaka mmoja. Mengi katika haya masomo yanaweza kupanuliwa na kufundishwa kwa muda mrefu, au kwa madarasa zaidi.

## 2. Mwongozo Wa Mwanafunzi

Kitabu hiki cha Mwongozo wa Mwanafunzi chaweza kutimiza makusudi mawili. Unaweza kutaka wanafunzi wasome kurasa husika katika kujiandaa kwa ajili ya somo linalofuata. Au, unaweza kuwataka wakisome baada ya wewe kufundisha somo, ili kufanya kama marudio na kuwa kama njia ya kusisitiza na kukazia kilichofundishwa darasani.

Tunakutia moyo uwaambie wanafunzi wajiandikie notsi darasani, hata ingawa utawapa Mwongozo Wa Mwanafunzi. Wanayojiandikia wenyewe pamoja na mazungumzo na mijadala darasani vitawasaidia sana kuelewa vizuri baadhi ya mada zinazoshughulikiwa katika Mwongozo Wa Mwanafunzi.

## 3. Mwongozo Wa Somo

Mazoezi yaliyo katika Mwongozo wa Somo yameandaliwa ili kumpa mwanafunzi kazi ya kufanya nje ya darasa. Baadhi ya kazi-mradi hizo zinasaidia kumwandaa mwanafunzi kwa ajili ya somo la darasa linalofuata.

Mengi ya mazoezi haya yamekusudiwa kuwasaidia wanafunzi wajikite ndani zaidi na kutazama baadhi ya maswala yanayojadiliwa darasani kwa kina. Lengo kuu la kazi hizo nyingi ni kuwaasaidia wanafunzi wagundue njia za kufanyia kazi hizo za kweli za Biblia katika maisha yao ya kila siku.

## 4. Mtihani Wa Mwanafunzi na Funguo la Majibu ya Mtihani

Mitihani hii imeandaliwa ili kutoa kipimo rahisi tu cha maendeleo ambayo kila mwanafunzi alipata katika uelewa wa kweli za Biblia zinazoshughulikiwa katika somo hili. Karatasi ya Majibu kwa ajili ya mtihani husika iko mara tu baada ya ukurasa wa mwisho wa ile nakala mfano ya mtihani wa mwanafunzi, katika Mwongozo huu wa Mwalimu.

## 5. Cheti Cha Somo

Cheti cha somo ni kwa ajili ya kuwatambua wale wanaomaliza kazi yote inayotakiwa kwa ajili ya somo hili na kufaulu mtihani. Mfano wa cheti hicho cha somo upo katika ukurasa wa mwisho wa kitabu hiki cha Mwongozo wa Mwalimu. Cheti cha Kufuzu pia kinapatikana kwa wale wanafunzi wanaomaliza masomo yote 14 katika mfululizo huu wa *Mafunzo ya Vikundi Ya Maisha Mapya*. Pia, mfano upo katika kile kitabu kinachoitwa ***Kuwatambulisha waalimu kwa Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya***.

# Jinsi Masomo Haya Yalivyotokea

Sulemani alisema, hakuna kitu kipya chini ya jua. Maneno hayo yanaweza kufaa hata kuhusu masomo haya. Mawazo yake mengi si mapya. Tunataka kutoa shukrani zetu maalum kwa Institute in Life Principles (Taasisi Ya Kanuni Za Maisha) kwa ushawishi mkubwa katika maisha ya watu waliotayarisha masomo haya. Masomo mengi yana alama za huduma hiyo ya Institue in Life Principles.

Nataka pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa walimu wengi sana na maelfu ya Wakristo wapya ambao wametumia masomo haya katika kipindi cha miaka kadhaa iliyopita. Mawazo yao yamekuwa na mchango mkubwa sana katika maandalizi ya masomo haya.
Pia ninamshukuru sana Ndugu Don Wilkerson kwa kunipa nafasi ya kufanya kazi katika kituo cha huduma ya Teen Challenge pale Brooklyn, New York, tokea mwaka wa 1971 hadi 1975. Katika miaka hiyo ndipo matayarisho yalipoanza ya masomo haya yaitwayo *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya*.

Toleo la tano la *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* lilitayarishwa kwa msaada wa kamati ya Mitaala ya huduma ya Teen Challenge Marekani. Natoa shukrani maalum kwa wote waliosaidia katika mapitio na marekebisho hayo.

# Sera Kuhusu Kunakili Machapisho Haya

Vitabu vya Mwalimu na kila kitu cha mwanafunzi kinachohusiana na masomo haya ya *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* kinalindwa na Sheria za Haki Miliki. Mpango maalum umefanywa ili kufasiri masomo haya kwa lugha hii ya Kiswahili. Masomo haya yanaweza kuchapwa na kugawanywa kwa ajili ya matumizi katika huduma za Teen Challenge na zinazofanana nazo, katika makanisa ya mahali fulani, shule na mashirika mengine na hata watu binafsi. Pia, yanaweza kupatikana kwenye mtandao kwa tovuti hii: www.iTeenChallenge.org Lakini, yasiuzwe. Yatolewe bure. Kwa wanaotaka kuchapisha na kuuza, wapate ruhusa kwa maandishi kutoka kwa Global Teen Challenge.

Dave Batty

# Pendekezo Kuhusu Mpangilio Wa Kufundisha

Somo hili ni moja kati ya 14 katika mfululizo wa *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya*. Masomo yote 14 yameorodheshwa hapa kama pendekezo la jinsi ya kuyafundisha. Mfuatano huu ulitayarishwa kwa ajili ya ufundishaji endelevu wa masomo haya. Tunaweza kuutazama kama picha ya gudurumu lenye vyuma kumi na vinne. Masomo haya hayategemei linalotangulia. Kila somo linasimama lenyewe. Basi, mwanafunzi anaweza kujiunga na madarasa wakati wowote na akaingia tu vizuri kwenye mfumo.

1. Nawezaje Kujua Mimi Ni Mkristo?
2. Kuitazama Biblia Kwa Haraka
3. Mtazamo
4. Majaribu
5. Maisha Ya Kikristo Yenye Mafanikio (ni pamoja na mafunzo juu ya huduma ya Roho Mtakatifu.)
6. Kukua kupitia kufeli
7. Matendo Ya Kikristo (Mahusiano Katika Kanisa La Mahali)
8. Utiifu kwa Mungu
9. Utiifu kwa Mwanadamu
10. Hasira na Haki za Kibinafsi
11. Jinsi Ya Kujifunza Biblia
12. Kujipenda na Kujikubali Mwenyewe
13. Mahusiano yako wewe Binafsi na Wengine
14. Nguvu Ya Kiroho na Mambo Yasio Ya Kawaida

Tazama kitabu kiitwacho, ***Kuwatanguliza waalimu kwa Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya***, ili kupata maelezo zaidi juu ya kufundisha masomo hayo.

# Mipangilio ya Masomo

# Kwa Mwalimu

Angalia ukurasa wa 4 wa Mwongozo wa Mwalimu kwa habari zaidi
kuhusu matumizi ya mipangilio hii ya masomo

# Maelezo ya jumla ya kozi

1. Siku moja au mbili kabla ya kipindi cha kwanza darasani, unaweza kutanguliza kozi hii kwa wanafunzi na kuwapa kazi zao za kwanza. Ikiwezekana wape Mwanafunzi Mwongozo wa Somo siku moja au mbili kabla ya kuanza kufundisha kozi hii. Wape wnafunzi Mwongozo wa Mwanafunzi na uwaambie wasome Sura ya Kwanza, ambayo itajadiliwa katika kipindi cha kwanza darasani.

2. Kwa ukurasa utakaofuatao katika mwongozo huu wa mwalimu kuna nakala ya *Orodha ya kazi za Darasani* inayotoa tarehe ambayo kila kazi inapaswa kukamilishwa. Waagize kujaza tarehe zinazofaa kwa nakala tupu kwenye *Orodha ya kazi za Darasani* nyuma ya Mwongozo wao.

3. Wajulishe wanafunzi kwamba wanapaswa kukamilisha Zoezi la 1 na Zoezi la 2 katika Mwongozo wa Somo kabla ya kikao cha kwanza cha darasa. Unaweza kuwaelezea kwa kifupi Zoezi la 2. Zoezi hili linasema watambue haja au hamu ambazo shetani alikuwa anajaribu kuwafanya watimize katika maisha yao walipokuwa kwa majaribio. (Angalia maswali ya 4 & 5 kwenye Zoezi la 2.) Tutajadili suala hilo katika kikao cha darasa la kwanza.

   Waambie ikiwa hawaelewi kile wanachopaswa kutoa kama majibu wanaweza kuwaacha pengo. Wanaweza kumaliza sehemu hiyo ya Zoezi la 2 wakati wa kipindi cha darasa la kwanza au baadaye. Hata hivyo, wanapaswa kukamilisha maswali matatu ya kwanza kwenye mifano yote katika Zoezi la 2 kabla ya kipindi cha darasa la kwanza.

4. **Kuendelea na somo baada ya darasa.** Njia rahisi ya kuwasaidia wanafunzi wako kuimarisha mafundisho muhimu ya kila somo ni kutengeneza mabango madogo kwa kutumia kompyuta yako, au kwa mkono.

   Kwa mfano:

   - ➪ Maelezo ya majaribu
   - ➪ Hatua sita za kushinda majaribu
   - ➪ Jinsi ya kujiandaadhidi ya majaribu
   - ➪ Mistari mikuu inayohusika na majaribu: 2 Timotheo 2:22, Zaburi 37:4-5, Yakobo 4:7-8, nk.
   - ➪ Taarifa muhimu kama vile: Matokeo ya kuingia katika majaribu ni yepi?

   Mwishoni mwa kila kipindi cha darasa, mwalimu mmoja anaweza kumpa mwanafunzi yeyote anayetaka mabango haya madogo. Wanafunzi mara nyingi watayaweka kwenye chumba chao cha kulala katika eneo la kusomo, au hata kuwapa familia zao. Kwa njia hii mafundisho muhimu ya kipindi cha darasa yanaendelea kukumbukwa na mwanafunzi na wengine wanapoyaona.

# Orodha ya kazi za Darasani

**Mada ya Somo:** Majaribu

**Chemsha Bongo** Mstari wa kumbukumbu — Tarehe

1. 1 Wakorintho 10:13 — Siku ya 2
2. Yakobo 4:7-8 — Siku ya 3
3. Hatua 6 za kushinda majaribu — Siku ya 4

**Zoezi** Tarehe ya Kuwasilisha

1. Siku 1
2. Siku 1
3. Siku 2
4. Siku 2
5. Siku 3
6. Siku 3 au 4
7. Siku 3 au 4
8. Siku 4

**Mtihani** Tarehe Siku 5

1

# Somo la 1
## Kuwa na Ufahamu wa Mahitaji Yangu

**1. Kweli Kuu ya Kibiblia**

Ninapaswa kufahamu mahitaji katika maisha yangu ambayo Shetani ananijaribia ili nifuata njia yake.

**2. Mstari Mkuu: Wafilipi 4:19 Biblia Takatifu (SUV)**

Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kadiri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu.

**3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili**

Sura ya kwanza ya mwongozo wa wanafunzi inaenda pamoja na somo hili. Zoezi la 1"*Majaribu katika Biblia,*" na Zoezi la 2, "*Kutambua majaribu yangu.*" katika Mwongozo wa somo litatumika katika somo hili.

**4. Zoezi la utangulizi wa somo (Dakika 5)**

Ili kutanguliza somo hili, waambie baadhi ya wanafunzi kujibu swali hili.

Fikiria kwa dakika moja kwamba wewe ni Adamu au Hawa katika Bustani ya Edeni. Unajua Mungu aliuweka mti mmoja bustanini na kusema hawawezi kula matunda yake. Sote tunajua Adamu na Hawa walikula tunda na kutupwa nje ya bustani. Kama ungekuwa Adamu au Hawa, ungefanya nini kuhusu mti huo mmoja?

**5. Jadili Hoja A, Majaribu ni nini?**
**(Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 4-5**

Taja tofauti kati ya majaribu yanayo jenga (kwa kawaida huitwa mtihani) na majaribu ya kutenda dhambi—ambayo yana uharibifu ikiwa Mkristo atayakubali. Toa mifano kadhaa ya kila aina ya majaribu, kisha ueleze kwamba katika kozi hii nzima tutajadili majaribu ya kutenda dhambi, sio majaribu ya kujenga au ya mtihani.

**6. Bango la majaribu**

Tengeneza bango lenye maelezo yafuatayo ya majaribu na uliweke darasani ili uweze kulirejelea katika kozi nzima. Maelezo haya yanatoka kwa ukurasa wa 4 wa Mwongozo wa Mwanafunzi.

**Majaribu**

**Wakati shetani anajaribu kukufanya uvunje sheria za Mungu ili kutimiza mahitaji au haja katika maisha yako.**

Shughuli nyingine unayoweza kuwaambia wanafunzi wako wafanye ni kutengeneza bango la picha ya baadhi ya sehemu ambazo Shetani anatujaribu ilitutendedhambi. Wanafunzi wanaweza kukata picha na maneno kutoka kwa matangazo ya magazeti.

**7. Jadili Hoja B, Je, majaribu yanaendanaje na maisha ya Mkristo? (Dakika 5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 5**

Chukua dakika chache kuelezea mahali pa majaribu katika maisha ya Mkristo. Wanapaswa kuelewa kwamba majaribu ni sehemu moja tu ya maisha ya Mkristo.

Hawapaswi kuangalia kila hali katika maisha kama fursa ya kujaribiwa kutenda dhambi. Siku zingine wanaweza kukumbana na majaribu mengi, na siku zingine, hawatakuwa na majaribu yoyote. Kama Wakristo waliokomaa, lazima tufanye mengi kila siku kuliko kupigana na majaribu.

**8. Ni nani anayetujaribu ili tutende dhambi? (Dakika 5)**

Jadili suala la ni nani anayetujaribu ili tutende dhambi. Waache watumie maandiko na majibu waliyoandika kwa swali la 1 na 2 kwenye Zoezi la 1 la Mwongozo wa Somo kuhusu ***Majaribu***.

1. **Je, Mungu huwajaribu watu kutenda dhambi? (Yakobo 1:13)**
2. **Ni nani huwajaribu watu kutenda dhambi?**
   **(Ni nani aliyemjaribu Yesu atende dhambi?) Soma Mathayo 4:1-11.**

**9. Jadili Hoja C, Je, Shetani alikufanya kutenda hilo? (Dakika 3-5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 6)**

Sisitiza umuhimu wa wajibu wa kibinafsi katika kufanya chaguzi za jinsi wanavyokidhi mahitaji na haja katika maisha yao.

Unaweza kutumia kielelezo kilichotolewa katika ukurasa wa 6 katika Mwongozo wa Mwanafunzi kuhusu kulinganisha “milango” ambayo Mungu na Shetani waliweka mbele yako. Toa mifano kadhaa ya milango tofauti ambayo Mungu na Shetani wanaweza kuweka mbele ya wanafunzi wako kutimiza mahitaji fulani waliyonayo.

**10. Shetani anakujaribu vipi? (Dakika 3-5)**

Taja kwamba Shetani mara chache huja na kusema, “Hujambo, Mimi ni Shetani, na ninakujaribu kutenda dhambi.” Anakuletea wazo kwamba atakusaidia kukidhi mahitaji katika maisha yako. “Una hitaji? Unahitaji nguo mpya nzuri. Hapa kuna njia rahisi ya kupata nguo hizo. Ziibe wakati makarani wa duka wanazungumza na watu wengine.”

1

**11. Majaribu ya Yesu (Dakika 10-15) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 9-10**

Jadili majaribu matatu ambayo Yesu alikabiliana nayo na mahitaji ambayo Shetani alikuwa anajitolea kuyakidhi maishani mwake. Tazama Mathayo 4:1-11. Waambie wanafunzi warejelee majibu yao kwa swali la 7 Zoezi la 1 kwenye Mwongozo wa Somo.

## Wakati Yesu alijaribiwa ili kutenda dhambi

Majaribu matatu yalikuwa majaribio ya Shetani kumfanya Yesu kukidhi mahitaji tofauti na haja katika maisha Yake.

**Jaribu la 1 – kugeuza mawe kuwa mkate.** Mathayo 4:2–4

Hitaji - Yesu alikuwa na njaa ya kimwili. Alihitaji chakula.

Tamaa - Thibitisha una uwezo wa kukidhi mahitaji maishani mwako. Thibitisha unaweza kufanya muujiza.

**Jaribu la 2 – ruka kutoka juu ya hekalu.** Mathayo 4:5–7

Tamaa - thibitisha kwamba unamwamini Mungu.

Tamaa - thibitisha kwamba Mungu atakutetea.

**Jaribu la 3 – Shetani anampa Yesu udhibiti wa ulimwengu wote**
Mathayo 4:8-10

Baada ya kutazama falme zote za ulimwengu, Shetani anataka kumpa Yesu yote hayo ikiwa atasujudu na kumwabudu.

Hitaji – kamilisha kazi yake ya kushinda (kushinda) ulimwengu kwa njia rahisi (kinyume na njia ya Mungu, ambayo hatimaye itasababisha kifo chenye uchungu cha Yesu msalabani).

*Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 9-10*

**12. Jadili Hoja D, Mahitaji katika maisha yako yanaendanaje na majaribu? (Dakika 5-15) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 7-8**

Hakikisha wanafunzi wako wameaanza kuelewa tofauti kati ya majaribu na mahitaji. Hitaji ni jambo halisi. Ikiwa mtu hajala, ana haja ya kimwili ya chakula. Majaribu ya Shetani ya kuiba chakula fulani ni njia moja ya kukidhi hitaji hilo. Kila jaribu linafungamanishwa na hitaji au tamaa uliyonayo. Wakati mwingine huenda usifahamu mahitaji yako.

Sasa unaweza kuwa wakati mzuri wa kujadili orodha ya mahitaji katika ukurasa wa 7 na 8 kwenye Mwongozo wa Mwanafunzi. Taja kwamba sote tuna mahitaji haya. Toa mifano kadhaa ya majaribu na mahitaji maalum. Onyesha jinsi Mungu atawasaidia wanafunzi wako kukidhi mahitaji haya katika maisha yao. Shetani pia atajaribu kuwasaidia kukidhi mahitaji haya.

**13. Jadili Hoja E. Mahitaji yako maishani yanaendanaje na majaribu? (Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 8-11**

Wasaidie wanafunzi wako kuona kwamba si kila jaribu linavutia haja katika maisha yako. Baadhi ya majaribu yanalenga hamu zetu. Baadhi ya hamu hizi zinaweza kuwa tamaa nzuri sana—kuona jina letu linalindwa, kutaka viatu vipya nk.

Tamaa zingine ni dhambi—ubinafsi, kuwaumiza wengine kwa tamaa kama ile ya kulipiza kisasi. Njia rahisi ya kujua kama tamaa yako ni dhambi ni kuangalia ni nini kitatokea ikiwa utafuata tamaa hiyo. Ikiwa tendo hilo ni dhambi, basi tamaa hiyo ni hamu ya dhambi.

Kwa mfano, ikiwa unataka kufanya mapenzi na mwanaume au mwanamke ambaye tayari amefunga ndoa na mtu mwingine—tamaa hiyo ni tamaa ya dhambi. Tamaa ya kuwa na mahusiano ya kimapenzi na jinsia tofauti sio tamaa ya dhambi. Lakini tunapozingatia tamaa hiyo kwa mtu ambaye tayari ameolewa, basi ni matumizi ya dhambi kwa tamaa hiyo.

Kama wewe ni mtu aliye funga ndoa, sio dhambi kuwa na tamaa ya kufanya mapenzi na mume au mke wako. Hata hivyo, ni dhambi kwako kutamani kufanya mapenzi na mtu mwingine yeyote ikiwa umeolewa.

Kwa mtu ambaye hajaolewa, ni kawaida kuwa na tamaa ya kuhusiana kimapenzi na mtu wa jinsia tofauti. Hata hivyo, Biblia inasema wazi sana kwamba kutimiza tamaa hizo, na kuendelea na kufanya mapenzi na mtu mwingine kabla ya ndoa ni kuvunja sheria za Mungu.

Maandiko mawili yanasaidia sana katika mjadala huu.

**2 Timotheo 2:22 Bibilia Takatifu (SUV)**

**Lakini zikimbie tamaa za ujanani; ukafuate haki, na imani, na upendo, na amani, pamoja na wale wamwitao Bwana kwa moyo safi.**

Mungu anaweka wazi kwamba hatupaswi kukubali kila tamaa kama jambo nzuri kwa sababu tuna tamaa hiyo katika mioyo yetu. Hii inakwenda kinyume na kile utamaduni wetu mara nyingi husema. Utamaduni wetu unawahimiza watu kufuata tamaa zao. Na Mwenyezi Mungu anaweka wazi kuwa baadhi ya matamanio hayapaswi kutimizwa. Hata zaidi, Mungu hasemi tupuuze tu tamaa hizi. Anatuambia “tukimbie tamaa hizi mbaya” na kisha kufuata “haki, imani, upendo na amani, pamoja na wale wote wanaomwita Bwana kwa moyo safi.”

**2 Wakorintho 10:5 Biblia Takatifu (SUV)**

**Tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu; na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo.**

Hapa Neno la Mungu linatupatia mfano wazi wa jinsi tunavyopaswa kukabiliana na kila tamaa—bila kujali ni aina gani ya tamaa. Ikiwa hamu hiyo iko dhidi ya mafundisho ya Neno la Mungu, basi tunapaswa kuibomoa kutoka kwa maisha yetu. Jambo la pili ni kwamba tunapaswa kuteka kila wazo—kila tamaa —na kuifanya kumtii Kristo.

1

Tamaa zisizodhibitiwa hakika zitasababisha vitendo vinavyoleta matatizo katika maisha yetu. Tamaa zisizodhibitiwa zinaweza kusababisha kwa urahisi dhambi. Neno la Mungu linaweka wazi kwamba tuna jukumu na uwezo wa kuchagua jinsi ya kukabiliana na kila tamaa katika maisha yetu. Mungu atatupatia nguvu tunayohitaji kukabiliana na tamaa hizi ipasavyo kwa kwa njia inayomtukuza.

Taja kwamba Shetani anataka tukubali tamaa zetu kwa shauku—ikiwa inahisi vizuri kufanya hivyo! Mungu anataka tutathmini tamaa zetu na kwanza kufikiria matokeo ya kutimiza tamaa hiyo. Ikiwa kitendo kitasababisha dhambi, basi Neno la Mungu linaweka wazi kwamba tunapaswa kukimbia kutoka kwa tamaa hiyo, kubomoa tamaa hiyo, au kuiteka na kuifanya imtii Kristo.

**14. Kuelewa tofauti kati ya mahitaji na tamaa**
**(Dakika 3-5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 7-11**

Wanafunzi wengi wana wakati mgumu kuelewa tofauti kati ya mahitaji na tamaa. Nenda kwenye orodha ya mahitaji kuanzia ukurasa wa 7 wa Mwongozo wa Mwanafunzi na uchukue baadhi ya mahitaji na utoe mifano ya mahitaji na tamaa zinazohusiana na kila kitu.

Kwa mfano, ***unahitaji*** chakula. Lakini unaweza ***kutamani*** *sundae fudge* kubwa ya ambayo ni moto.

***Unahitaji*** koti wakati wa baridi, hasa ikiwa kuna theluji nje. Lakini unaweza ***kutamani*** kuwa na makoti 7 au 8. Unaweza ***kutamani*** kuwa na koti ndefu la ngozi.

***Unahitaji*** kuwa na marafiki, lakini unaweza ***kutamani*** mtu fulani awe rafiki yako, hasa ikiwa yeye ni tajiri, au ana sura nzuri sana!

Inaweza kuwa bora kwa wanafunzi wako kuandika ufafanuzi wa mahitaji na tamaa. Waambie wakuambie kuhusu kile kinachopaswa kujumuishwa katika fasili hizi. Unaweza kuunda bango la ufafanuzi huu na kuliweka kwenye ukuta wa darasa lako kwa marejeleo ya kozi hii nzima. Hapa kuna fasili zilizopendekezwa.

**Hitaji** - kitu tunachotakiwa kuwa nacho ili kuwa na kudumisha maisha kwa uwezo wake kamili.

**Tamaa** - kitu tunachotaka kuwa nacho, lakini si lazima tuwe nacho.

Baada ya kutoa ufafanuzi wa maneno haya mawili, unaweza kuchukua muda na kuwawezesha wanafunzi kuunda orodha ya mahitaji na tamaa. Weka mifano yao chini ya kila mada. Unaweza kuweka orodha hizi kwenye karatasi kubwa ambazo unaweza kuweka kwenye ukuta wa darasa lako ili uweze kurejelea orodha hizi katika kozi hii yote. Itakuwa vyema kuendelea kuongeza mifano ya ziada kwenye orodha hizi unapofundisha kozi hii yote.

1

**15. Jinsi Shetani anavyovutia mahitaji na tamaa zako (Dakika 5-10)**

Taja kwamba jaribu moja linaweza kuwa jaribio la Shetani kukusaidia kukidhi mahitaji mawili au matatu na /au tamaa katika maisha yako. Kwa mfano, jaribu la kwanza la Shetani kwa Yesu jangwani lililenga haja ya Yesu ya chakula. Shetani pia alijaribu kumfanya Yesu aamini kwamba alihitaji kuthibitisha kwamba Alikuwa Mwana wa Mungu. Shetani alijaribu kuweka hamu kwa Yesu ili kuthibitisha ukweli huu.

Shetani anaweza kujaribu kukushawishi kwamba kile ambacho ni tamaa kweli ni haja katika maisha yako. "Kwa kweli unahitaji koto jipya la ngozi, au gari hilo jipya, au marafiki zako hawatakupenda."

Njia nyingine ambayo Shetani anajaribu kukuondoa kutoka kwa mpango wa Mungu kwako ni kukufanya utimize haja au hamu ambayo haikubaliani na wakati wa Mungu. "Kuridhika mara moja" ni jambo la kawaida sana katika maisha ya wale ambao wamekuwa wakijihusisha na ulevi. Lakini pia inaweza kuwa tatizo kwa maisha ya mtu yeyote. "Kuridhika mara moja" kunaweza kuwa jaribu lililofungwa kwa haja, kama ilivyokuwa kwa jaribu la kwanza ambalo Yesu alikabiliana nalo katika Mathayo 4:2-4.

**16. Jinsi Shetani alivyomjaribu Hawa (Dakika 5-10)**

Unaweza pia kujadilina na wanafunzi kuhusu mahitaji (ya kweli, hamu) ambayo Shetani alisema itatimizwa ikiwa Hawa atakula matunda ya mti katika Bustani ya Edeni. Waambie wasome Mwanzo 3 ili kupata njia halisi ambayo Shetani alisema Hawa angefaidika kama angefanya kile alichomwambia afanye.

**17. Angalia majaribu yetu (Dakika 5-15)**

Tumia vielelezo kadhaa vya majaribu ambayo wewe na/au wanafunzi wako mmekumbana nayo hivi karibuni. Waache wanafunzi watoe baadhi ya mifano waliyoandika kwenye Zoezi 2 la Mwongozo wa Somo, "Kutambua majaribu yangu." Jadili mahitaji au tamaa ambazo Shetani alikuwa anamjaribu kutimiza kwa njia yake. Unaweza pia kufafanua ni sheria gani za Mungu ambazo ungevunja ikiwa ungeenda kwa njia hii ya Shetani.

**18. Kutendea somo kazi kibinafsi (Dakika 5-10)**

Zingatia matumizi binafsi kwa kujifunza jinsi ya kutambua mahitaji na/au tamaa ambazo Shetani anajaribu kukufanya utimize wakati anakujaribu kutenda dhambi. Ikiwa hawajafanya hivyo tayari, waache wanafunzi wako wajaze majibu ya maswali 3 & 4 katika mifano waliyoweka kwenye Zoezi la 2 la Mwongozo wa Somo. Unaweza kuwaacha wanafunzi kwanza watoe majibu kibinafsi kwa maswali haya. Kisha waingie katika makundi ya watu 3 au 4 na kujadili majibu yao.

**19. Kazi**

A. Sahihisha Mwongozo wa Somo Zoezo la 1, *“Majaribu katika Biblia.”*

B. Angalia ili kuona kwamba wamekamilisha Zoezi 2 la Mwongozo wa Somo, *“Kutambua majaribu yangu.”* Watahitaji Zoezi la 2 kukamilisha Zoezi la 5 ambalo linatoka kwa kipindi cha tatu cha darasa. Unaweza kuangalia Zoezi la 2 na kulirejesha atika kipindi cha darasa lifuatalo.

C. Eleza Zoezi la 4 la Mwongozo wa Somo, *“Jinsi wahusika wa Biblia walivyoshughulikia majaribu yao.”* Kama unavyoona, wanafunzi wana njia mbalimbali mbadala wanazoweza kuchagua. Unaweza kuhakikisha kwamba wanafunzi wote hawachagui jombo moja, hasa kama unataka kutumia haya katika majadiliano ya darasa katika kipindi kijacho. Tazama Mpangilio wa Somo la 2, kipengee cha 4, katika ukurasa wa 19 wa Mwongozo wa Mwalimu.

D. Eleza kwamba Zoezi la 3 la Mwongozo wa Somo, *“Mahitaji na tamaa yangu,”* limeundwa kufuatilia somo mlilolimaliza. Wako huru kutumia maelezo yao ya darasani na Mwongozo wa Mwanafunzi ili kukamilisha kazi zao kwenye Zoezi hili. Utaamua kile unachotaka wafanye na *“Maswali ya kusoma Zaidi,”* katika ukurasa wa 2 wa Zoezi. Unataka waandike majibu ya maswali haya kwenye karatasi tofauti na wakupe ili usahihishe?

E. Waache wanafunzi wasome Sura ya 2 katika Mwongozo wa Mwanafunzi ili kujitayarisha kwa kipindi kifuatacho cha darasa.

**20. Tathmini ya somo**

Hebu andika mawazo yako kuhusu jinsi ya kuboresha somo hili.
Ni sehemu zipi zilizokuwa nzuri?
Ni sehemu zipi ambazo wanafunzi wamepata shida kuzielewa?
Ni sehemu zipi zilizokuwa za msaada sana kwa wanafunzi wako?

# Somo la 2
## Kuyashinda Majaribu

2

**1. Kweli Kuu ya Kibiblia**

Ninapaswa kukariri na kutumia mfano wa Kibiblia wa kukabiliana na majaribu.

**2. Mstari mkuu: Waefeso 6:13 Biblia Takatifu (SUV)**

Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote, kusimama.

**3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili**

Sura ya 2 kwenye Mwongozo wa Mwanafunzi inaenda sambamba na somo hili. Zoezi la 4 kwenye Mwongozo Somo, "*Jinsi wahusika wa Biblia walivyoshughulikia majaribu yao*." pia litatumika katika somo hili.

**4. Zoezi la utangulizi wa somo: "Unasimama wapi?"**
**(Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 12**

Anza darasa kwa kujadili suala lililoibuliwa katika ukurasa wa 12 kwenye Mwongozo wa Mwanafunzi, Hoja A. "*Unasimama wapi*?" Chora picha ya ukuta kwa ubao au kupitia kwa projekta yako kuonyesha uamuzi unaokabili kila Mkristo. Katika upande mmoja wa ubao weka, "*Kujitolea kikamilifu kufuata njia ya Mungu*." Kwa upande mwingine wa ubao weka, "*Kujitolea kikamilifu kufuata njia ya Shetani.*"

Sasa weka kwa picha hii wahusika kadhaa wa Biblia wanaojulikana. Unaweza kuwaacha wanafunzi kuwaweka watu waliowasoma walipokuwa wakifanya Zoezi 4 la Mwongozo wa Somo. Mifano ya Agano la Kale ya Yusufu na Danieli na marafiki zake watatu itakuwa kwenye upande wa, " *Kujitolea kikamilifu kufuata njia ya Mungu*."

Yezebeli na Ahabu wa Agano la Kale watakuwa upande mwingine. Yuda pengine angekuwa juu ya ukuta na mshale akielekea kufuata njia ya Shetani. Petro, wakati wa kusulubiwa kwa Yesu, alikuwa amegeuka kuelekea kwenye njia ya Shetani, kisha akatubu na kugeuka kufuata njia ya Mungu.

Taja kwamba hawawezi kutembea kwenye ukuta kwa maisha yao yote. Kila Mkristo lazima afanye uamuzi wa kumfuata Mungu au Shetani. Kusisitiza umuhimu wa uamuzi huu katika uhusiano wake na mafanikio ya kushinda majaribu ya dhambi.

**5. Jinsi wahusika katika Biblia walivyokabiliwa na majaribu (Dakika 10-15)**

Jadili wahusika tofauti kwenye Biblia ambao wameorodheshwa kwenye Zoezi la 4 katika Mwongozo wa Somo. Angalia jinsi walivyopinga majaribu waliyokumbana nayo. Jaribu kutoa sababu ni kwa nini mtu alishindwa, alipoingia kwenye majaribu.

**6. Jadili Hoja C. Je, ni hatua gani za kushinda majaribu?**
**(Dakika 10-15) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 13-17**

Sasa kwa haraka wasilisha hatua sita za kuyashinda majaribu. Taja kwamba huu ni utaratibu ambao wanaweza kuutumia katika kukabiliana na majaribu ya dhambi.

2

## Hatua sita za kuyashinda majaribu

1. Fahamu kuwa unajaribiwa
2. Sema "HAPANA" kwa majaribu
3. Anza kuzungumza na Mungu
4. Jiulize, "Shetani anajaribu kutimiza mahitaji yapi?"
5. Tafuta njia ya Mungu ya kutoka kwa majaribu haya
6. Weka malengo ambayo yatakusaidia kutimiza mahitaji yako kwa njia ya Mungu

***Imenukuliwa kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 13-17***

Baada ya kutanguliza orodha nzima kwenye ukurasa wa 14 katika Mwongozo wa Mwanafunzi, toa mfano jinsi unavyoweza kutumia muundo huu kwa jaribu moja maalum.

Kisha urudi nyuma na ujadili kila hatua kwa undani. Angalia kurasa za 14-17 katika Mwongozo wa Mwanafunzi kwa maelezo zaidi juu ya kila hatua. Jaribu kutoa mifano kadhaa ya jinsi wanaweza kutumia kila hatua kwa majaribu tofauti. Unaweza kuwaambia wanafunzi watoe mifano ya majaribu kutoka kwa kazi waliyoifanya kwenye Zoezi la 2 kwenye Mwongozo wa Somo.

**7. Tofautisha kati ya mahitaji na majaribu (Dakika 5-10)**

Unapojadili majaribu tofauti, jaribu kutenganisha ***majaribu*** kutoka kwa ***mahitaji*** ili waweze kuona jinsi muundo huu wa kibiblia utawasaidia kuyashinda majaribu na wakati huo huo kutimiza hitaji ambalo Shetani anavutia.

Unaweza pia kutaja sheria ya Mungu ambayo mtu huyu atavunja ikiwa ataingia katika majaribu ya Shetani.

**8. Shughuli ya iwapo ningekuwa Mungu au Shetani (Dakika 10-20)**

Shughuli hii ndogo ya kikundi imeundwa ili kuwafanya wanafunzi wako kuangalia pande zote mbili za majaribu—upande wa Mungu na upande wa Shetani.

Piga chapa au nakilisha kila seti ya maagizo kwenye ukurasa tofauti wa karatasi. Utakipa kila kikundi upande mmoja tu wa majaribu. Kundi A litashughulikia upande wa "**Kama ningekuwa Mungu**" upande wa majaribu. Kundi lingine litashughulikia upande wa "**Kama ningekuwa Shetani**" upande wa majaribu hayo.

Baini ni majaribu gani utakayotumia kwanza katika darasa lako. Ikiwa darasa unalofundisha halikabiliani na majaribu yaliyoorodheshwa hapa chini, basi badilisha mifano hii. Tumia majaribu ambayo ni ya kawaida kwa washiriki wengi wa darasa lako.

Kwa shughuli hii, utagawa darasa kwa vikundi vidogo vidogo vya watu 2 hadi 4 kwa kila kikundi. Jaribu kuwa na idadi sawa ya watu kwenye vikundi (vikundi vya 2, 4, 6, nk)

A. Kipe kila kikundi karatasi moja yenye maelekezo juu ya "*Ningekuwa Mungu... au Shetani...*" Elezea maagizo na kisha uwape takribani dakika 5 ili kukamilisha kazi zao.

B. Acha kila kikundi kiripoti kwa darasa zima jinsi wangewashawishi Wakristo kupinga au kuingia kwenye majaribu.

C. Waagize wanafunzi wengine kusikiliza mawasilisho ya kila kikundi kana kwamba wao ndio wanajaribiwa.

D. Baada ya kusikiliza pande zote mbili za majaribu, waache wanafunzi wajadili ni upande gani ulikuwa wa ushawishi zaidi—wa Mungu au wa Shetani? Acha waeleze ni sehemu gani za hoja zilikuwa na ushawishi zaidi na kwa nini. Unaweza pia kujadili ni kwa nini baadhi ya hoja hazikuwa na ushawishi zaidi.

E. Unaweza kuwaambia wanafunzi watoe maoni yoyote ya ziada jinsi njia ya Mungu au shetani inaweza kuboreshwa. Taja katika majadiliano kwamba Shetani na Mungu wanaweza kujaribu kukuvuta kwa mahitaji au hamu inayohusika na majaribu.

## Shughuli ya kama ningekuwa Mungu au Shetani

**1A. Kama ningekuwa Mungu**

Kama ningekuwa Mungu, hivi ndivyo ningekushawishi usidanganye kwenye mtihani wako shuleni.

Maelekezo kwa kikundi chako: Andika mambo 5-10 ambayo ungesema au kufanya kujaribu kumshawishi kufuata ushauri wako.

**1B. Kama ningekuwa Shetani**

Kama ningekuwa Shetani, hivi ndivyo ningekushawishi kudanganya katika mtihani wako shuleni.

Maelekezo kwa kikundi chako: Andika mambo 5-10 ambayo ungesema au kufanya kujaribu kumshawishi afuata ushauri wako.

**2A. Kama ningekuwa Mungu**

Kama ningekuwa Mungu, hivi ndivyo ningekushawishi usivute bangi ili kukubaliwa na marafiki zako.

Maelekezo kwa kikundi chako: Andika mambo 5-10 ambayo ungesema au kufanya kujaribu kumshawishi kufuata ushauri wako.

**2B. Kama ningekuwa Shetani**

Kama ningekuwa Shetani, hivi ndivyo ningekushawishi kuvuta bangi ili kukubaliwa na marafiki zako.

Maelekezo kwa kikundi chako: Andika mambo 5-10 ambayo ungesema au kufanya kujaribu kumshawishi kufuata ushauri wako.

**3A. Kama ningekuwa Mungu**

Kama ningekuwa Mungu, hivi ndivyo ningekushawishi kuwatii wazazi wako.

Maelekezo kwa kikundi chako: Andika mambo 5-10 ambayo ungesema au kufanya kujaribu kumshawishi kufuata ushauri wako.

**3B. Kama ningeikuwa Shetani**

Kama ningekuwa Shetani, hivi ndivyo ningekushawishi kutowatii wazazi wako.

Maelekezo kwa kikundi chako: Andika mambo 5-10 ambayo ungesema au kufanya kujaribu kumshawishi kufuata ushauri wako.

**9. Kutendea somo kazi kibinafsi (Dakika 5)**

Kwa matumizi ya kibinafsi leo, waache wanafunzi wafanye kazi ya kukariri mpangilio wa hatua sita unazoweza kutumia wakati wa kukabiliana na majaribu (ukurasa wa 14 Mwongozo wa Mwanafunzi). Waambie ni lini watafanya mtihani. Angalia *Orodha ya Kazi za Darasani* kwa tarehe ya mtihani huu. Wahimize kuanza kutumia mpangilio huu wa majibu leo. Sisitiza umuhimu wa kuanza kwa hatua ya kwanza. Ikiwa wana wakati mgumu kukumbuka kutumia hatua moja, wahimize angalau kuandika orodha ya majaribu yote waliyokutana nayo leo. Hii ni njia moja ya kujenga ufahamu wa majaribu yako.

**10. Kazi**

A. Mwishoni mwa kipindi cha darasa, toa mtihani juu ya 1 Wakorintho 10:13.

B. Sahihisha Ziezi la 3 Kwenye Mwongozo wa Somo, *“Mahitaji na tamaa yangu,”* na Zoezi la 4, *“Jinsi wahusika wa Biblia walivyoshughulikia majaribu yao.”*

C. Ikiwa ulikusanya Zoezi la 2 kwenye Mwongozo wa Somo katika kipindi cha mwisho cha darasa, warejeshee wanafunzi leo. Eleza jinsi Zoezi la 5 linavyokwenda sambamba na Zoezi la 2.

D. Kama bado hujafanya uamuzi, unapaswa kuwajulisha wanafunzi wako ni zoezi gani wanapaswa kukamilisha kabla ya kipindi kifuatacho cha darasa. Ikiwa unapanga kutumia Zoezi la 6 kwenye Mwongozo wa Somo, *“Kutumia muundo mpya kukabiliana na jaribu,”* na Zoezi la 7, *“Ziara ya kibinafsi na mtu maarufu katika Biblia,”* kwa kipindi kifuatacho cha darasa, basi wafahamishe ili waweze kuwa na kazi inayohitajika na iliyokamilika kwa wakati.

E. Waache wanafunzi wako wasome Sura ya 3 katika Mwongozo wa Mwanafunzi ili kujitayarisha kwa kipindi chetu kifuatacho cha darasa.

**11. Tathmini ya somo**

Hebu andika mawazo yako kuhusu jinsi ya kuboresha somo hili.
Ni sehemu zipi zilizokuwa nzuri?
Ni sehemu zipi ambazo wanafunzi wamepata shida kuzielewa?
Ni sehemu zipi zilizokuwa za msaada sana kwa wanafunzi wako?

# Somo la 3
## Kujitayarisha kwa Majaribu



1. **Kweli kuu ya Kibiblia**

   Kama Mkristo, ninapaswa kujitayarisha mwenyewe ili niweze kufanikiwa kushinda kila majaribu.

2. **Mstari Mkuu: 1 Wakorintho 10:13 Biblia Takatifu (SUV)**

   Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili.

3. **Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili**

   Sura ya 3 katika Mwongozo wa Mwanafunzi inaenda sambamba na somo hili. Zoezi la 2 kwenye Mwongozo wa Somo, "*Kutambua majaribu yangu*," na Zoezi la 5, "*Mtazamo mpya wa majaribu ya zamani*," linaweza pia kutumika kwa somo hili.

4. **Maandalizi ya mwalimu kwa kipindi hiki cha darasa**

   Pengine jambo moja nzuri ambalo unaweza kufanya ili kujiandaa kwa somo hili ni kupitia jaribu moja au mawili kwa kutumia Zoezi la 6 katika Mwongozo wa Somo, "*Kutumia muundo mpya kukabiliana na jaribu*," na Zoezi la 8, "*Kujiandaa kwa majaribu*," kama mfano wako. Ili kufanya somo hili liwe lenye mafanikio ni kufahamu mambo kutokana na uzoefu wako wa kujitayarisha kwa majaribu.

5. **Zoezi la utangulizi wa somo (Dakika 5)**

   Unaweza kuwaacha baadhi ya wanafunzi kusimulia jinsi walivyotumia mpangilio mpya wa kukabiliana na majaribu ambao tulitanguliza kwenye somo la pili katika Mwongozo huu wa Mwalimu. Jambo hili lilijadiliwa katika Sura ya 2 kwenye Mwongozo wa Mwanafunzi. Ikiwa unafikiri wanafunzi wako hawataweza kutoa majibu yao ya kibinafsi hivi mwanzoni mwa darasa, kuwa tayari kutoa mfano moja au miwili kutoka kwa maisha yako mwenyewe, au wanafunzi wa zamani.

6. **Njia ya kimsingi inayohitajika kukabiliana na majaribu (Dakika 5)**

   Chukua dakika chache hapa kusisitiza umuhimu wa kujiandaa kuyashinda majaribu. Kuna njia nne kuu ambazo wanafunzi wako wanazihitaji kukua ikiwa watafanikiwa kujitayarisha na kuyashinda majaribu ya kutenda dhambi.

   A. Kuwa na uwezo wa kutambua majaribu mara tu yanapoanza.

   B. Kuwa na uwezo wa kutathmini hali hiyo na kuamua ***Hitaji*** au ***tamaa*** ambayo Shetani anajaribu kuwafanya watimize.

C. Kuwa na uwezo wa *kugundua* njia ya Mungu ya kutimiza mahitaji na tamaa zao, na kisha kufuata njia ya Mungu.

D. Njia nyingine yenye manufaa ni kuweza kufahamu matokeo ya kufuata njia ya Mungu au njia ya Shetani wakati wa majaribu. Hii inaweza kukusaidia sana katika kumhimiza mtu kufuata njia ya Mungu.

**7. Jadili Hoja A, Mkaribie Mungu**
**(Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 18-19**

Jadili umuhimu wa kumkaribia Mungu kama njia kuu ya kujitayarisha kwa majaribu. Tumia hii kama fursa ya kucheleza na kuangalia kwa mapana maisha ya Kikristo. Majaribu yatakuja na kupita katika maisha yetu yote. Hata hivyo hoja hii ni pahali pazuri pa kuanza kwa kujitayarisha kwa majaribu—kuanza na kumkaribia Mungu.



Itakuwa vizuri pia kusisitiza jinsi mahusiano bora yalivyo muhimu katika kujitayarisha kukabiliana na majaribu. Kwa njia moja hivi ni vita vya kiroho, na Shetani ni adui mwenye nguvu. Tukijaribu kupigana na majaribu ya Shetani kwa nguvu zetu wenyewe—sisi wenyewe---mara nyingi tutashindwa na vita. Lakini wakati tunakuwa sehemu ya jeshi—jeshi la Mungu—basi mafanikio ni jambo la uhakika.

Tunapaswa kuwa na uhusiano wa karibu na Mungu ili kuweza kupigana na majaribu. Lakini pia tunapaswa kuwa na mahusiano ya karibu na Wakristo wengine ambao wanaweza kutusaidia tunapokabiliwa na majaribu. Pia ni sehemu muhimu sana ya maisha yenye afya. Tunapokuwa na mahusiano mazuri na Wakristo wengine, tuna fursa bora za kukidhi mahitaji yetu kwa njia ya kimungu—na hivyo kupunguza nguvu ya majaribu ya kutenda dhambi.

**8. Jadili Hoja B, Timiza mahitaji yako kwa njia za Mungu**
**(Dakika 10-20) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 19-22**

Jadili masuala muhimu yaliyoibuliwa katika Hoja B, “*Timiza mahitaji yako kwa njia za Mungu*.” Hakikisha kuwa una mifano kadhaa au visa tayari kutumia katika majadiliano ya darasa. Unaweza kuwaambia wanafunzi warejelee baadhi ya majaribu waliyoorodhesha kwenye Zoezi 2 la Mwongozo wa Somo, “*Kutambua majaribu yangu*,” na Zoezi la 5, “*Mtazamo mpya wa majaribu ya zamani*.” Chukua muda darasani kuwaonyesha jinsi ya kutumia Biblia ili kujua njia ya Mungu ya kutimiza hitaji fulani au tamaa fulani.

Jaribu kuwasaidia wanafunzi kutathmini kwa makini kazi waliyoifanya kwenye Zoezi la 2 kwenye Mwongozo wa Mwanafunzi, hasa kwa maswali ya 4 & 5 kwa kila mfano. Angalia ikiwa wamefahamu vyema mahitaji halisi au tamaa zinazoambatana na kila jaribu.

Je, wameonyesha tu haja ya kumpinga ibilisi, au wamekwenda zaidi na kushughulika na mahitaji halisi na tamaa katika maisha yao ambayo Shetani anavutia?

Rejelea ukurasa wa 7 Kwenye Mwongozo wa Mwanafunzi kwa orodha ya kina ya mahitaji katika maisha yetu.

**9. Tambulisha Hoja ya C, “Mwache Mungu aamue tamaa nzuri.”**
**(Dakika 3-5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 22-24**

Unapotanguliza hatua hii, hakikisha kwanza wanaelewa tofauti kati ya tamaa na hitaji. Vielelezo kadhaa katika hatua hii vitasaidia.

Unaweza kurejelea Hoja 12-15 kwenye mpangilio wako wa somo la kwanza (kurasa 14-17 kwenye Mwongozo wa Mwalimu) kwa maelezo ya ziada juu ya tofauti kati ya mahitaji na tamaa. Kujadili suala hili tena ni muhimu sana kwa wanafunzi wako. Hakikisha wanafunzi wako wanaelewa jinsi ya kutumia habari hii katika maisha yao ya kila siku.

Katika kujadili hoja ndogo 1, **“Fahamu kile Mungu anapenda”**, waache wanafunzi watambue baadhi ya tamaa za Mungu ambazo tunapaswa kuwa nazo. Unaweza kuwapa baadhi ya maandiko kuangalia ikiwa hawawezi kutoa hoja nyingi. Angalia ukurasa wa 22-23 katika Mwongozo wa Mwanafunzi kwa baadhi ya maandiko unayoweza kutumia hapa.

**10. Jadili Hoja C-2, Ondoa tamaa za zamani za dhambi**
**(Dakika 5-15) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 23-24**

Waache wanafunzi waorodheshe tamaa za dhambi wanazopaswa kutupilia mbali. Sisitiza umuhimu wa kufanya zaidi ya kutupilia mbali tamaa hizi za zamani. Lazima wazibadilishe na tamaa za Mungu ikiwa wanataka kuwa na utulivu wa kweli katika safari yao ya Kikristo.

Unaweza kuwaacha baadhi ya wanafunzi kuelezea darasa jinsi waliweza kuondoa tamaa ya dhambi za zamani.

Baadhi ya wanafunzi wako wanaweza kuwa wameharibiwa sana na dhambi ya mtu mwingine dhidi yao—kwa mfano, dhulma ya kimapenzi. Mwanafunzi wako anaweza kuwa na hisia kali za hasira dhidi ya mtu huyu, na anataka kulipiza kisasi. Chukua muda kuwaeleza wanafunzi wako jinsi wanavyoweza kumgeukia Mungu kwa suala la kulipiza kisasi. Ikiwa wameshikilia ghadhabu na hasira, itawaharibu wenyewe zaidi ya mtu mwingine.

Badala ya kueleza jinsi watakavyolipiza kisasi, eleza jinsi wanavyoweza kukumbuka akilini mwao njia nzuri ya kukabiliana mtu aliyewakosea. Suala hili linaweza pia kushughulikiwa chini ya Hoja D, “*Majaribu mengine yanaweza kuzuiwa*.”

**11. Jadili Hoja C-3, Tumia maadili ya biblia kupima tamaa zako**
**(Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 24**

Suala hili la maadili ya kibiblia linaweza kuwa gumu kwa wanafunzi wako kuelewa, kulingana na ukomavu wao wa kiroho. Wasaidie kuelewa kwamba baadhi ya tamaa zinapaswa kupuuzwa. Kwa msaada wa Mungu tunaweza kusema, “Ninachagua kutoipa tamaa kipaumbele maishani mwangu.”

**12. Jadili Hoja D, Majaribu mengine yanaweza kuzuiwa**
**(Dakika 10-20) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 25-26**

Katika kujadili mada, "*Majaribu mengine yanaweza kuzuiwa*," hakikisha una mifano ya wazi ya kuonyesha jambo hili. Unaweza kuwaambia baadhi ya wanafunzi kutoa mifano ya jinsi wanavyoweza kuzuia majaribu fulani.

**13. Mfano wa Zoezi la 8 Mwongozo wa Somo (Dakika 10-20)**

Kabla ya mwisho wa kipindi cha darasa, unaweza kujadili mojawapo ya majaribu kwenye Zoezi la 8 Mwongozo wa Somo, "*Kujiandaa kwa majaribu*." Hii itawasaidia kujua jinsi ya kukamilisha kazi kwenye zoezi hili ambalo watakuwa wanafanya baada ya kipindi cha darasa la leo.



**14. Jadili Hoja E: Jihadhari na mikakati ya Shetani**
**(Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 26-27**

Mara nyingi Wakristo wapya wanachanganyikiwa na mikakati inayotumiwa na Shetani. Chukua muda wa kujadili baadhi ya mikakati ambayo Shetani anatumia, mengine yameorodheshwa katika Mwongozo wa Mwanafunzi kwenye kurasa za 26-27. Unaweza kuongeza mengine.

Hakikisha umefafanua kwamba ikiwa majaribu yatarudi, yanaweza kuwa ishara ya kitu zaidi ya kimoja. Yanaweza kuwa ishara kwamba hawako karibu na Yesu. Tumia Yakobo 4:7-8 kushughulikia suala hili.

Lakini kuna nyakati ambapo majaribu yanarudi na sio ishara ya kuanguka kiroho. Chukua muda kujadili Luka 4:13 na 2 Wakorintho 11:14 inayohusiana na majaribu ya Shetani.

**15. Kutendea somo kazi kibinafsi (Dakika 5-10)**

Matumizi binafsi ya somo hili yatazingatia kila mwanafunzi kuchukua jaribu fulani na kukamilisha Zoezi la 8 kwenye Mwongozo wa Somo , "*Kujiandaa kwa majaribu.*" Hawatafanya hivyo darasani. Wahimize wanafunzi kujaribu kutumia kile walichojifunza wanapokabiliana na majaribu ya kutenda dhambi.

**16. Kazi**

A. Sahihisha Zoezi la 2 kwenye Mwongozo wa Somo "*Kutambua majaribu yangu*," na Zoezi la 5, "*Mtazamo mpya wa majaribu ya zamani*," ikiwa haujasahihisha.

B. Sahihisha Zoezi la 7 kwenye Mwongozo wa Somo, "*Ziara ya kibinafsi na mtu maarufu katika Biblia.*"

C. Mwishoni mwa kipindi cha darasa, toa mtihani juu ya Yakobo 4:7-8.

D. Waache wanafunzi wako wasome Sura ya 4 katika Mwongozo wa Mwanafunzi katika maandalizi ya kipindi kifuatacho cha darasa.

### 17. Tathmini ya somo

Hebu andika mawazo yako kuhusu jinsi ya kuboresha somo hili.
Ni sehemu zipi zilizokuwa nzuri?
Ni sehemu zipi ambazo wanafunzi wamepata shida kuzielewa?
Ni sehemu zipi zilizokuwa za msaada sana kwa wanafunzi wako?

# Somo la 4
## Kukabiliana na Kufeli

**1. Kweli kuu ya Kibiblia**

Ninapaswa kujifunza kukabiliana na kufeli kwangu kwa njia ambayo itanisaidia kumkaribia Mungu.

**2. Mstari Mkuu: Waebrania 4:15-16 Biblia Takatifu (SUV)**

15Kwa kuwa hamna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi. 16Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.

4

**3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili**

Sura ya 4 katika Mwongozo wa Mwanafunzi inaenda sambamba na somo hili. Zoezi la 4 kwenye Mwongozo wa Somo, "*Jinsi wahusika wa Biblia walivyoshughulikia majaribu yao*," na Zoezi la 7, "*Ziara ya kibinafsi na mtu maarufu katika Biblia*," inaweza pia kutumika kwa somo hili.

**4. Zoezi la utangulizi wa somo: Maoni mawili ya kufeli (Dakika 5)**

Mwanzoni mwa somo la leo, taja kwamba kuzungumza juu ya kufeli hakupaswi kutazamwa kama kukubali. Mkristo ambaye anataka kufuata njia ya Mungu kwa kawaida hatatenda dhambi na kusema mwenyewe, "Oh, hiyo ni sawa. Mwenyezi Mungu atanisamehe nikimwomba." Mungu hataki tuanguke kwa majaribu. Tunapaswa kuwa na mtazamo ule ule ambao Mungu anao.

Lakini kwa upande mwingine, wengi wetu huingia katika majaribu mara kwa mara. Madhumuni ya somo hili ni kuangalia baadhi ya sababu za kufeli na kuangalia matokeo ya kufeli kwetu. Pia tutaangalia kile Mkristo anpaswa kufanya anapofeli.

Kushindwa kuyashinda majaribu hakumaanishi mtu anapoteza wokovu wake wakati huo. Hakuna hata mmoja wetu aliye mkamilifu, lakini sote tunaweza kuwa waaminifu kwa kufanya bidii yetu kupinga majaribu. Tunaposhindwa, tunahitaji kuwa waaminifu, kukiri, na kusimama imara ili kufanya vyema wakati ujao tutakapokutana na majaribu hayo.

**5. Jadili Hoja A, Ni nini kinachotokea unapoingia kwenye majaribu? (Dakika 10-15) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 28-32**

Waambie wanafunzi wako kukupa maoni yao juu ya suala hili, **"Ni nini kinachotokea unapoingia kwenye majaribu?"** Chukua muda ili wanafunzi watoe baadhi ya mifano ya matokeo baada ya kuanguka kwa majaribu.

Utaamua ni muda gani utatumia kwa kila moja ya matokeo 12 yaliyo katika sehemu hii. Hata hivyo, kuwa makini kwa hoja ndogo A-9, ***"Kutoa mwongozo wa busara wa kile kinachofaa na kisichofaa."*** Wengi wetu tumejifunza jinsi ya kuhalalisha dhambi zetu zilizopita. Kwa kuwa sisi ni Wakristo, hatutapoteza mara moja "utaratibu wa kuhesabiwa kama wenye haki." Kwa kweli, tunaweza kupata kuwa ni rahisi sana kuhalalisha dhambi ndogo. Hii inaibua umuhimu wa kuzifanya upya akili zetu, na kuona kila jaribu kwa mtazamo wa Mungu.

Hoja ndogo ya 9 pia inajadili suala la "kufanya moyo wako kuwa mgumu." Elezea kwa makini jinsi ilivyo rahisi kuifanya mioyo yetu kuwa migumu ikiwa tutakataa na kupuuza wakati Mungu anatuhukumu kutokana na dhambi zetu. Tunaporuhusu urazini kukua katika maisha yetu, inakuwa rahisi sana kuifanya mioyo yetu kuwa migumu.

4

Chukua muda pia kuangalia yaliyotokea kwenye baadhi ya hadithi za Biblia katika Mazoezi ya 4 na7 katika Mwongozo wa Somo. Chagua wale unaohisi watakuwa na manufaa zaidi kwa wanafunzi wako.

**6. Jadili Hoja B, Kwa nini watu huingia kwa majaribu? (Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 32-35**

Tumia mifano hiyo hiyo ya kibiblia kutoka kwa Zoezi la 4 kwenye Mwongozo wa Somo, ***"Jinsi wahusika wa Biblia walivyoshughulikia majaribu yao***," na Zoezi la 7, ***"Ziara ya kibinafsi na mtu maarufu katika Biblia,"*** katika kujadili ni kwa nini watu huingia katika majaribu. Kukiwa na mifano mingi ya kibiblia unaweza tu kubahatisha kile kinachoweza kuwa sababu, kwa kuwa Biblia haielezi sababu ya ni kwa nini waliingia kwenye majaribu.

Pia waache wanafunzi wako watoe mifano yao ya kibinafsi ya kuingia katika majaribu. Kuwa makini sana kuchunguza mifano wanayotumia, hasa ikiwa darasa lako lina wanaume na wanawake. Kujadili maelezo maalum ya majaribu ya kufanya mapenzi katika mpangilio huo labda sio jambo zuri. Hata kama ni darasa la jinsia moja, unapaswa kuwa makini kuhusu maelezo ambayo yanatolewa, kwani hata majadiliano ya maelezo haya yanaweza kusababisha mawazo yasiyo mazuri kwa wanafunzi wako.

Njia moja ya kushughulikia jambo hili ni kuchagua mifano kutoka kwa wanafunzi mapema—kwa kutumia mifano waliyokuwa wameweka kwa kazi zao kwa darasa hili na kutumia mifano inayofaa bila kutaja majina ya wanafunzi wanaohusika.

**7. Tathmini ya wanafunzi ya kufeli kwao kwa zamani (Dakika 5-15)**

Waache wanafunzi watathmini jaribu moja au mawili katika maisha yao wenyewe ambalo liliwaangusha. Je, wanaweza kutambua sababu ya kuanguka? Huenda kukawa na mambo kadhaa yaliyochangia kufeli kwao. Linaweza kuwa jambo la busara ikawa watarejelea baadhi ya majaribu waliyotumia katika mazoezi kwenye Mwongozo wa Somo kwa kozi hii.

Taja umuhimu wa kufahamu sababu waliyoitoa. Hii inaweza kuwasaidia kujua watakapoanzia wakijiandaa kwa majaribu ya baadaye.

**8. Jadili Hoja C, Unapaswa kufanya nini baada ya kushawishiwa na jaribu? (Dakika 10-15) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 35-37**

Hakikisha umejadili kile mtu anapaswa kufanya baada ya kuanguka katika majaribu. Baada ya kujadili masuala tofauti katika sehemu hii, wahimize kutumia mawazo haya wakati wao wa ibada wanapoomba juu ya majaribu yoyote yaliyowaangusha hadi siku hiyo.



**9. Jinsi Mungu alivyokabiliana na watu katika Biblia ambao walimfeli (Dakika 5-10)**

Katika kujadili kile mtu anapaswa kufanya baada ya kuanguka katika majaribu, unaweza kuangalia jinsi baadhi ya wahusika wa Kibiblia walivyokabiliana na kushindwa kwao. Daudi na Petro walikiri dhambi zao. Yuda hakufanya hivyo. Unaweza pia kujadili majibu ya Mungu kwa mtu anayekiri dhambi zake. Daudi alikuwa bado mfalme, na Petro aliendelea kuwa kiongozi mkuu wa kanisa.

**10. Kuapa kutoshindwa tena (Dakika 5)**

Waambie wanafunzi wako kwamba wasiape kwa Mungu baada ya kuingia kwa majaribu. Wakristo wengine wanaweza kufikiri kwamba kuapa ni jibu zuri la kiroho, “Mungu, niliingia katika majaribu haya. Ninaahidi kwamba sitaingia katika majaribu hayo tena.” Kiapo hiki kina jukumu ndogo la kukusaidia kutatua tatizo halisi. Ibilisi pia anaweza kutumia hii kama njia ya kuleta hukumu kubwa juu ya mtu baada ya kufeli tena katika siku zijazo.

Ikiwa unataka kuapa kwa Mwenyezi Mungu, itakuwa vyema kusema, “Mungu, ninataka kuapa Kwako kuwa nitakukaribia kila siku. Pia ninaahidi kutumia muda _____ kwa wiki ijayo kusoma kila Unachosema kuhusu jaribu hili na jinsi ninavyoweza kukabiliana nalo kwa njia inayokupendeza.”

Aina hii ya ahadi ni rahisi sana kuweka, na kwa muda mrefu na zaidi itaenda sambamba na kuendeleza uhusiano wa karibu na Mungu.

**11. Kutendea somo kazi kibinafsi (Dakika 5-10)**

Zingatia matumizi ya kibinafsi juu ya kuwa waaminifu kwa Mungu kuhusu kushindwa kwao. Wanahitaji kukiri dhambi zao haraka. Pia wanapaswa kutafuta njia za kujifunza kutokana na kushindwa kwao. Kushindwa huku kunapaswa kuwasaidia kuona mahali wanapaswa kujitayarisha vyema kwa majaribu ya baadaye.

**12. Kazi**

A. Sahihisha Zoezi la 8 kwenye Mwongozo wa Somo, "*Kujiandaa kwa majaribu*." Unaweza kuwataka wanafunzi wako wajibu swali la 7 kabla ya kukusanya kazi yao. Ikuwa itakuwa lazima, baadhi ya wanafunzi wanaweza kuhitaji siku kadhaa zaidi kukamilisha Zoezi, kulingana na wakati wanapokabiliwa na majaribu waliyotumia kwenye Zoezi lao.

B. Mwishoni mwa kipindi cha darasa, toa mtihani juu ya hatua sita za kushinda majaribu.

### Hatua sita za kuyashinda majaribu

1. Fahamu kuwa unajaribiwa
2. Sema "HAPANA" kwa majaribu
3. Anza kuzungumza na Mungu
4. Jiulize, "Shetani anajaribu kutimiza mahitaji yapi?"
5. Tafuta njia ya Mungu ya kutoka kwa majaribu haya
6. Weka malengo ambayo yatakusaidia kutimiza mahitaji yako kwa njia ya Mungu

***Imenukuliwa kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 14***



**13. Tathmini ya somo**

Hebu andika mawazo yako kuhusu jinsi ya kuboresha somo hili.
Ni sehemu zipi zilizokuwa nzuri?
Ni sehemu zipi ambazo wanafunzi wamepata shida kuzielewa?
Ni sehemu zipi zilizokuwa za msaada sana kwa wanafunzi wako?

# Somo la 5
## Mtihani

**1. Utangulizi**

Fanya utangulizi wa somo litakalofuata.

A. Wape Mwongozo wa Somo au Mazoezi yoyote ambayo yanapaswa kukamilishwa kabla ya kipindi cha kwanza cha kozi ifuatayo utakayofundisha.

B. Waelekeze wanafunzi kufungua ukurasa wa mwisho katika Mwongozo wa Somo Lipya. Wanapaswa kupata nakala safi ya ***Orodha ya Kazi za Darasani.*** Wape tarehe za majaribio ya chemsha bongo, Zoezi, na mtihani.

C. Wape Mwongozo wa Mwanafunzi mpya na uwaambie kurasa watakazosoma kabla ya kipindi kifuatacho darasani.

**2. Wape mtihani wa Somo hili.**

**3. Ikiwa hujafanya hivyo bado, rudisha chemsha bongo zote na mazoezi ambayo umesahihisha.**

# Mwongozo wa Mwanafunzi

Mwongozo wa Mwanafunzi Haujajumuishwa kwenye hati hii,
lakini unapatikana katika hati tofauti.

Tafadhali angalia ukurasa wa 5 ya Mwongozo huu Wa Mwalimu kwa habari kuhusu matumizi ya Mwongozo wa Mwanafunzi.

# Mwongozo wa Somo

Haukujumuishwa kwenye hati hii, lakini unapatikana katika hati tofauti.

.

Tafadhali angalia ukurasa wa 5 ya Mwongozo huu Wa Mwalimu kwa habari kuhusu matumizi ya Mwongozo wa Somo.

# Mtihani

# Majibu ya mtihani

# Cheti cha Somo

Tazama ukurasa wa 5 wa mwongozo huu kwa habari zaidi kuhusu matumizi ya mtihani na cheti.

**Jina**___________________________ **Majaribu**

**Tarehe**_________________________ **Mtihani wa Toleo la 5**

**Darasa**_________________________ __________**Gredi**

## Maswali ya Kweli au Si Kweli (Alama 1 kwa kila swali)

**Maelekezo:** Weka alama ya ____X_____ ikiwa jibu ni kweli.

Weka alama ya ____O_____ ikiwa jibu si kweli.

1._______ Ukimpinga shetani, ataacha kukujaribu na kukukimbia.

2._______ Njia bora ya kujiandaa kwa jaribu ni kumkaribia Mungu.

3._______ Baada ya kuwa Mkristo, Mungu anataka upuuze tamaa zako.

4._______ Yesu hakujaribiwa kwa bidii kama watu wanavyojaribiwa leo hii.

5._______ Shetani siku zote anataka nifikirie juu ya matokeo ya mwisho ya kufanya kile ananijaribu nifanye.

6._______ Mungu ameahidi kutimiza mahitaji yako yote.

7._______ Shetani anapowashawishi watu watende dhambi, huwaambia kuwa anawajaribu.

8._______ Mungu anawaamuru Wakristo waachane na tamaa za dhambi.

9._______ Hakuna kitu ambacho Mkristo anaweza kufanya kuzuia jaribu lolote kutoka kwa shetani.

10._______ Wakati watu wanashindwa na jaribu, kawaida hupata kuridhika kwa muda na kufurahishwa na kile wanachofanya.

11._______ Sipaswi kamwe kukimbia kitu kinachonishawishi kutenda dhambi.

12._______ Haijalishi unatumia muda gani kujiandaa kwa jaribu, Shetani bado atakushawishi utende dhambi.

13._______ Wakati mtu anashindwa na jaribu kawaida ni rahisi kuanguka katika kishawishi hicho hicho tena.

14._______ Mtu anapojaribiwa kutenda dhambi anapaswa kumlaani shetani mara moja.

15._______ Shetani kamwe hatajaribu kukufanya uhisi mwenye hatia kwa kukubali jaribu baada ya kukiri dhambi yako kwa Mungu.

16._______ Ikiwa nitajaza mahitaji yangu kwa njia za Mungu, Shetani hatakuwa na fursa nyingi za kunijaribu katika maeneo hayo.

17._______ Ni dhambi kujaribiwa.

### Maswali ya Kweli-Siyo Kweli (muendelezo )

18.________ Napaswa niongee na Mungu kila wakati ninapojaribiwa.

19.________ Ikiwa mtu ataruhusu tamaa zake zipite mipaka , basi vishawishi vya dhambi vinaweza kuwa vigumu sana kushinda.

20.________ Ni sawa kufikiria juu ya kufanya kile unachojaribiwa kufanya, ili usikifanye.

21.________ Baada ya kukubali jaribu fulani, unapaswa kuweka nadhiri kwa Mungu kwamba hautakubali tena kishawishi hicho tena.

22.________ Ninapojaribiwa kutenda dhambi, napaswa kujaribu kila mara kutafuta hitaji ambalo Shetani anajaribu kunifanya nikutane nalo.

### Maswali ya Kuchagua kati ya Majibu Mengi (Alama 3 kila moja)

Maagizo: Chagua jibu bora na uweke herufi ya jibu kwenye laini tupu mbele ya swali.

1.________ Njia bora ya kushinda majaribu ni

A. Kupuuza. (jiambie , "Hayapo.")

B. Tafakari juu ya mistari ya Biblia inayozungumzia kila jaribu.

C. Cheka jaribu.

2.________ Je, ni mara ngapi Mungu huwajaribu watu kutenda dhambi?

A. Ikiwa tu mtu ni mwenye dhambi.

B. Wakati mwingine mtu anapomwasi.

C. Kamwe Mungu hawajaribu watu .

### Maswali ya Majibu Mafupi

1. Jaribu ni nini? (Alama 6)

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

2. Je, ni mambo gani 6 unayoweza kufanya **kujiandaa** kwa jaribu?
(Alama 12, alama 2 kwa kila sehemu)

1.________________________________________

2.________________________________________

3.________________________________________

4.________________________________________

5.________________________________________

6.________________________________________

3. Mtu anapaswa kufanya nini (kufikiria) anapojaribiwa kutenda dhambi?
Orodhesha mpango wa hatua 6 uliojadiliwa darasani. (Alama 18, alama 3 kwa kila sehemu)

1.________________________________________

2.________________________________________

3.________________________________________

4.________________________________________

5.________________________________________

6.________________________________________

4. Kila wakati shetani anakujaribu utende dhambi, anajaribu kukufanya utosheleze hitaji moja au hamu moja maishani mwako. Eleza tofauti kati ya mahitaji yako na matakwa yako. (Alama 6)

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

5. Toa mifano 2 ya mahitaji na matamanio. Jaribu kuchagua zile ambazo shetani hutumia mara nyingi wakati anajaribu Wakristo kutenda dhambi.
(Alama 8, alama 2 kwa kila sehemu)

Tamaa______________________________

Tamaa______________________________

Haja______________________________

Haja______________________________

6. Je, Mkristo anapaswa kufanya nini baada ya kushawishiwa na jaribu?
Andika angalau mambo 4 ambayo Mkristo anapaswa kufanya.
(Alama 8, alama 2 kwa kila sehemu)

1. ______________________________
______________________________

2. ______________________________
______________________________

3. ______________________________
______________________________

4. ______________________________
______________________________

7. Andika mistari ya kukariri. (Alama 14, alama 7 kwa kila kifungu)

______________________________
______________________________
______________________________
______________________________
______________________________
______________________________
______________________________
______________________________
______________________________
______________________________
______________________________
______________________________
______________________________
______________________________

# Majaribu

## Mtihani Toleo La 5

## Karatasi Ya Majibu Kwa Ajili Ya Mwalimu

**Ukurasa Wa 1**
**Maswali Ya Kweli au Si Kweli**
(Kila swali lina alama 1 na nusu)

1. X Kweli
2. X Kweli
3. 0 Si Kweli
4. 0 Si Kweli
5. 0 Si Kweli
6. X Kweli
7. 0 Si Kweli
8. X Kweli
9. 0 Si Kweli
10. X Kweli
11. 0 Si Kweli
12. X Kweli
13. X Kweli
14. 0 Si Kweli
15. 0 Si Kweli
16. X Kweli
17. 0 Si Kweli

**Ukurasa Wa 2**

18. X Kweli
19. X Kweli
20. 0 Si Kweli
21. 0 Si Kweli
22. X Kweli

**Maswali ya Kuchaguo Kati ya Majibu Mengi** (alama 3 kila moja)

1. B
2. C

**Maswali ya Simulizi Fupi**

1. Alama 6

   Wakati Shetani anajaribu kukufanya uvunje sheria za Mungu ili kukidhi hitaji au hamu katika maisha yako.

# Majaribu
## Mtihani Toleo La 5
## Karatasi Ya Majibu Kwa Ajili Ya Mwalimu

### Ukurasa wa 3

2. Alama 12, alama 2 kwa kila sehemu
   (Yanatakiwa majibu 6 tu)

   Majibu yanayopendekezwa:

   1. Mkaribie Mungu
   2. Soma Biblia
   3. Tambua majaribu yako makubwa
   4. Fahamu hitaji ambalo Shetani anajaribu kukufanya utimize
   5. Fahamu njia ya Mungu ya kutimiza mahitaji yako
   6. Fanya ahadi ya kujaza mahitaji yako kwa njia ya Mungu
   7. Ondoa tamaa za zamani za dhambi
   8. Kuza matakwa ya Kimungu
   9. Tumia maadili ya biblia kupima tamaa zako
   10. Jifunze jinsi ya kuzuia vishawishi

3. Alama 18, alama 3 kwa kila sehemu

   1. Tambua unajaribiwa
   2. Sema “HAPANA” kwa majaribu
   3. Anza kuzungumza na Mungu
   4. Jiulize, “Shetani anajaribu kutimiza mahitaji yapi?”
   5. Tafuta njia ya Mungu ya kutoka kwa majaribu haya
   6. Weka malengo ambayo yatakusaidia kutimiza mahitaji yako kwa njia ya Mungu

4. Alama 6

   Majibu yanayopendekezwa:

   Hitaji ni kitu ambacho lazima uwe nacho katika kuishi maisha kamili na kamilifu.

   Tamaa ni kitu ambacho unataka, lakini unaweza kusihi bila kuwa nacho.

# Majaribu
## Mtihani Toleo La 5
## Karatasi Ya Majibu Kwa Ajili Ya Mwalimu

### Ukurasa wa 4

5. Alama 8, alama 2 kwa kila sehemu

   Majibu ya kibinafsi

6. Alama 8, alama 2 kwa kila sehemu  (Yanatakiwa majibu 4 tu)

   1. Kubali kufeli kwako
   2. Fahamu hitaji au hamu katika maisha yako, na ufanye mipango ya kulikamilisha kwa njia ya Mungu
   3. Tathmini kujitolea kwako kwa Kristo
   4. Dai ahadi za Mungu kwa nguvu
   5. Usijihukumu

7. Aya za kukariri

   Alama 14, alama 7 kwa kila mstari

   1 Wakorintho 10:13

   Yakobo 4:7-8

## Hongera

________________________________________

Amemaliza

# Majaribu

Tunatambua kujitoa kwako katika masomo haya na ni matumaini yetu kwamba kwa mafanikio utaendelea na masomo yako yajayo.

Wakufunzi ____________________________

Tarehe ________________________________

## Hongera

________________________________________

Amemaliza

# Majaribu

Tunatambua kujitoa kwako katika masomo haya na ni matumaini yetu kwamba kwa mafanikio utaendelea na masomo yako yajayo.

Wakufunzi ____________________________

Tarehe ________________________________